



## OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. HWT/L2/7/101

29.5.2024

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya Mkataba ili kuziba nafasi zilizo wazi kwa Kada ya udereva daraja la II.

**DEREVA DARAJA LA II NAFASI (05)****1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kuendesha gari la abiria na malori
- ii. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- iii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftali la safari.
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadili utakavyoelekezwa na msimamizi wako.

**1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe Mtanzania mwenye cheti cha kuzaliwa na kitambulisho au namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na leseni ya Udereva daraja E au C1
- iii. Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitano (5) bila kusababisha ajali.
- iv. Awe na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II au sifa nyingine inayolingana nayo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- v. Awe na umri wa **miaka 18** au zaidi.
- vi. Awe na afya njema, mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi ya udereva katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

## 2 NAMNA YA KUOMBA


- a. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Kijiji Cha Nyamwaga, Barabara ya Nyamwaga, S.L.P 16, Tarime-Mara, Simu +25528-2690518, Nukushi: +25528-2690144, Barua pepe: [ded@tarimedc.go.tz](mailto:ded@tarimedc.go.tz), Tovuti: [www.tarimedc.go.tz](http://www.tarimedc.go.tz).
- b. Maombi yote yatumwe na nakala za vyeti vya taaluma, mafunzo, cheti cha kuzaliwa, na Kitambulisho cha Taifa vilivyothibitishwa na Mahakama au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na Serikali.
- c. Testimonials' 'Provisional Results', Statement of Results; Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI**.
- d. Barua ya maombi iandikwe kwa mkoni na kwa lugha ya Kiswahili na kингereza tofauti na hapo maombi hayatapokelewa.
- e. Taarifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- f. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (detail CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.

### 3.0. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Maombi yatapokelewa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Nyamwaga, mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **13.06.2024** saa 9:30 alasiri.

Tunawakaribisha wote wenye sifa zilizotajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao kwa utaratibu ulioelekezwa. Maombi yote yatumwe kuitia anwani ya:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P 16,  
TARIME



Solomon I. Shati  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**TARIME**

*MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMAHURI YA WILAYA YA TARIME*

#### Nakala:

Tangazo hili lkinapatikana kwenye mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pamoja na kwenye tovuti ya Halmashari ya Wilaya ya Tarime ambayo ni: [www.tarimedc.go.tz](http://www.tarimedc.go.tz).